Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

# WANAKONDOA MJI

**TOLEO MAALUM**

MACHI 2024



## PONGEZI KWA DKT.SAMIA SULUHU HASSAN

## BILIONI 14.2 ZA MAFANIKIO KWA MIAKA MITATU

Baraza la Waheshimiwa Madiwani, Menejimenti, Watumishi na wananchi wa Halmashauri ya Mji Kondoa tunakupongeza kwa miaka mitatu ya mafanikio katika kuliongoza taifa.

Kazi Iendelee!

**Imeandaliwa na**
**Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali**
**Halmashauri ya Mji Kondoa**

## Bodi ya Uhariri

Ndg. Said M. Majaliwa
Ndg. Sekela Mwasubila
Ndg. Violencia Mbakile

## Mitandao ya Kijamii

Kondoatc

## Tovuti ya Halmashauri

www.kondoatc.go.tz

## Mawasiliano

S.L.P 711 Kondoa
Simu: + 255 712264912
Nukushi : +255262360313

## Kero Yako Wajibu Wangu

**Imeandaliwa na**
**Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali**
**Halmashauri ya Mji Kondoa**

## NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI



Ndg. Said Majaliwa
**Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondoa**

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hadi siku ya leo na kuniwezesha kusimamia utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Pili natoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Hassan kwa kutupatia fedha shilingi **Bilioni 14.2** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Tatu namshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Dkt. Khamis Mkanachi kwa kutuongoza vizuri katika kufanikisha miradi hii kwa kipindi chote hiki.

Miradi imetekelezwa katika sekta mbalimbali kama mchanganuo unavyoonyesha :

- Elimu Msingi **Bilioni 2.077**
- Elimu Sekondari **Bilioni 3.88**
- Afya Bilioni **2.99**
- Elimu bila malipo **Bilioni 1.942**
- TASAF **Bilioni 1.3** kwa ajili ya kusaidia kaya maskini ambapo walengwa **2784** wamenufaika .
- Utawala **Milioni 413.0**
- Mfuko wa Jimbo **Milioni 127.7**

Aidha fedha hizi zimesaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha na kuongeza miundombinu katika sekta zote ambapo imeboresha maisha ya wananchi kwani huduma muhimu zimesogezwa kwao.

**KAZI IENDELEE!!**

# VIONGOZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA



**Mhe. Mohamed Abdi Kiberenge**
**Mwenyekiti Halmashauri ya Mji Kondoa**



**Mhe. Dkt. Khamis Mkanachi**
**Mkuu wa Wilaya Kondoa**



**Ndg. Said Mwemezi Majaliwa**
**Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondoa**



**Mhe. Ally Juma Makoa**
**Mbunge wa Kondoa Mjini**

**Shukrani kwa viongozi hawa ambao kwa umoja wao wamefanikisha kupatikana kwa fedha zote na kuzisimamia kufikia mafanikio yanayoonekana.**



# MAFANIKIO SEKTA YA AFYA

## MILIONI 900 ZA UKARABATI WA HOSPITALI

Serikali kuu imeleta fedha kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali ya Mji ambapo kutokana na uchakavu wa majengo muhimu katika hospitali hiyo Halmashauri imejenga majengo mapya matatu ambayo ni jengo la kisasa la upasuaji, jengo la mama na mtoto lenye sehemu ya upasuaji ndani ya jengo na jengo la kuhifadhia maiti la kisasa.



## MILIONI 600 UNUNUZI WA VIFAA TIBA

Serikali imeleta fedha za ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa vyenye thamani ya shilingi **milioni 600** kwa ajili ya Hospitali ya Mji Vituo vya Afya na Zahanati ambapo imerahisisha upatikanaji wa huduma ambazo awali zilikuwa hazipatikani katika Hospitali ya Mji na vituo vya afya ikiwemo Kituo cha Afya Kingale.



## BILIONI 1.490 UJENZI WA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Kwa kipindi cha miaka mitatu Serikali imeleta shilingi **bilioni 1.490** kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 2 ambavyo ni Kituo cha Afya Kolo na Serya, ujenzi wa zahanati 4 katika mitaa ya Hachwi, Tampori, Mlua na Choka, ujenzi wa nyumba pacha za watumishi kituo cha Afya Serya na ujenzi wwananchi waliokuwa akitembea umbali mrefu kufuata huduma katika Hospitali ya Mji.



## MAPOKEZI YA MAGARI 2 DIVISHENI YA AFYA

Serikali imeleta gari la wagonjwa kwa ajili ya kurahisha huduma ya kuwapeleka wagonjwa wanaopata rufaa kwenda hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Dodoma na Hospitali ya Benjamini Mkapa. Gari hili lilikabidhiwa na Mbunge wa Kondoa Mjini Mhe. Ally Makoa kwa niaba ya serikali. Aidha Serikali imetoa gari kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya afya.



# MAFANIKIO SEKTA YA ELIMU MSINGI

## MILIONI 907.7 ZA GP LANES II NA BOOST

Kupitia mradi wa GP LANES na BOOST serikali imeleta zaidi ya shilingi **milioni 907** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ya awali na msingi katika Shule mbalimbali ikiwemo ujenzi wa shule mpya 1 ya Msingi. Ujenzi huu umesaidia sana kuongeza uandikishaji wa wanafunzi wa awali kwa kuwa madarasa yamejengwa kisasa kabisa.



## MILIONI 280 UKARABATI SHULE KONGWE

Serikali kwa kipindi cha miaka 3 imetoa shilingi **milioni 280** kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za Kolowasi na Kondoa kutokana na madarasa yake kuwa katika hali isiyoridhisha. karabati huo umesaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia walimu



## MILIONI 183.7 ZA MRADI WA UVIKO 19

Kwakipindi cha miaka mitatu Halmashauri imepokea **shilingi milioni 183.7** kupitia mradi wa UVIKO 19 ambapo fedha hizi zimetumika kujenga sehemu za wanafunzi kunawia mikono na kuchimba visima katika S/M Kilimani na Mongoroma pamoja na ujezni wa miundombinu ya kusambazia maji safi na salama na ujenzi wa madarasa

## MILIONI 124 ZA UJENZI WA MABWENI



Kwakipindi cha miaka mitatu Halmashauri imepokea shilingi **milioni 142.9** kupitia Mamlaka ya elimu Tanzania (TEA) na shilingi **milioni 128** kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 2 kwaajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Iboni. Lengo la mradi huu ni kuhamikisha watoto wote wenye mahitaji maalum wanapata elimu katika mazingira rafiki wakati wote.

## MILIONI 574.7 KWA AJILI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU

Serikali kwa kipindi cha miaka 3 imetoa shilingi **milioni 574.7** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwemo madarasa na nyumba 2 pacha za walimu katika S/M Hachwi na Chandimo pamoja na matundu ya vyoo.

# MAFANIKIO SEKTA YA ELIMU SEKONDARI



## BILIONI 1. ZA UJENZI SHULE 2 ZA SEKONDARI

Serikali kwa kipindi cha miaka 3 imetoa zaidi ya shilingi **bilioni 1** kwa ajili ya ujenzi wa Shule 2 mpya za Sekondari. Shule ya Sekondari Tura Day ilipewa **shilingi milioni 470** na Shule ta Bolisa Sekondari **shilingi milioni 544**. Ujenzi wa shule hizi umesaidia kuwapunguzia umbali wa kutembea wanafunzi wa kata ya Bolisa na Kondoa Mjini ikiwa ni pamoja na kupunguza msongamano wa wanafunzi wa Shule za Kondoa Mjini.



## MILIONI 601 ZA MABORESHO KONDOA GIRLS

Serikali kwa kipindi cha miaka 3 imetoa zaidi ya shilingi **Milioni 601** kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mapya 2 , ujenzi wa madarasa 8, ujenzi wa matundu 10 ya vyoo na utengenezaji wa vitanda na makabati. Miundombinu hiyo imesaidia kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 500 hadi zaidi ya 800.



## BILIONI 1.2 ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU

Serikali kwa kipindi cha miaka 3 imetoa zaidi ya shilingi **Bilioni 1.2** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, maabara, na matundu ya vyoo, nyumba pacha za walimu sehemu za kunawia mikono pamoja na uchimbaji wa kisima kirefu. Shule zilizonufaika ni pamoja na Bicha, Dilai, Serya, Ula, Kolo, Kwapakacha, Mtobubu, Gubali

## KUONGEZEKA KWA UFAULU KIDATO CHA NNE

Serikali kwa kipindi cha miaka 3 baada ya kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia imesaidia kwa kiwango kikubwa kuongoza asilimia ya ufaulishaji kwa wanafunzi kwa kidato cha nne kutoka asilimia .. hadi .. 2023 na kupelekea Halmashauri kupata tuzo ya mshindi wa pili kimkoa siku ya wadau wa Elimu.




## MAPOKEZI YA GARI LA DIVISHENI

Serikali kwa kipindi cha miaka 3 imetoa gari moja kwa ajili ya divisheni ya Elimu Sekondari kwa ajili ya kusaidia ufuatiliaji wa elimu katika shule zote kwa lengo la kuhakikisha ufaulu unaongezeka

# MAFANIKIO SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI











## UNUNUZI WA SCANNER YA UDONGO

Serikali ya awamu ya sita kwa kipindi cha miaka mitatu imefanikiwa kuleta scanner kwa ajili ya kupima udongo wa wakulima kabla ya kilimo bila gharama zozote kwa lengo la kuhakikisha kuwa wakulima wanalima kilimo cha uhakika na kuongeza uzalishaji. Na jumla ya sampuli 2600 za udongo zilichukuliwa na matokeo yamewanufaisha wakulima 7500 na zoezi linaendelea.

## MAPOKEZI YA TANI ZA MBOLEA YA RUZUKU

Kwa kipindi cha miaka mitatu Serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kuleta mbolea ya ruzuku na kuiuza kwa gharama nafuu kwa wakulima wa Halmashauri ya Mji Kondoa ambapo jumla ya tani 49 za mbolea ya kupandia na tani 15 za mbolea ya kukuzia zililetwa na kuuzwa kwa wakulima. Lengo la kuleta mbolea hizo ni kuhakikisha kila mkulima analima na kuzalisha chakula kwa uhakika zaidi.

## MAPOKEZI YA MAHINDI YA BEI NAFUU

Kwa kipindi cha miaka mitatu Serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kuleta mahindi kiasi cha **tani 600** na kuwauzia wananchi kwa gharama nafuu kutokana na chakula walichovuna kuwa kidogo na sokoni kuuzwa kwa bei kubwa.

## MAPOKEZI YA PIKIPIKI ZA MAAFISA UGANI

Kwa kipindi cha miaka mitatu Serikali ya awamu ya sita imefanikiwa kuleta pikipiki **21** kwa ajili ya Maafisa Ugani lengo ni kuhakikisha wakulima wanafikiwa katika maeneo waliyopo na kupata elimu ya kilimo na wanalima kwa tija.

# MAFANIKIO SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII




## MILIONI 295 ZATOLEWA MIKOPO YA ASIMILIA 10

Kwa kipindi cha miaka mitatu Halmashauri ya Mji Kondoa imefanikiwa kutenga na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi **milioni 295** kwa **vikundi 41** vya Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutoka asilimia kumi ya mapato yake. Makundi hayo yamenufaika ambapo kwasasa wengi wameweza kuboresha maisha yao kwa kujiajili na kuajili wengine kutokana na biashara wanazofanya. Aidha kiasi cha shilingi milioni **114.3** zimetengwa kwa ajili ya utoaji wa mikopo hiyo baada ya serikali kusitisha zoezi la utoaji wa mikopo kwa lengo la kuweka mkakati mzuri wa utoaji wa mikopo hiyo.




## MILIONI 43 USIMAMIZI WA HUDUMA NDOGO ZA KIFEDHA

Ili kuhakikisha wananchi wanapata unafuu katika mikopo itolewayo na taasisi mbalimbali za kifedha na watu binafsi (maarufu kausha damu). Serikali iliamua kukasimu madaraka ya usimamizi na ufuatiliaji wa taasisi hizo kwa Halmashauri ili kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.



Halmashauri imepokea shilingi **milioni 43** kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi ambapo imefanya ukaguzi wa taasisi hizo na kutoa ushauri penye mapungufu pamoja na mafunzo kwa wamiliki wa taasisi hizo, waheshimiwa madiwani na wanavikundi wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 na ununuzi wa vitendeakazi vya ofisi.

# HALI ILIVYOKUWA KABLA YA MABORESHO NA BAADA

## KABLA

## BAADA





Kushoto ni Zahanati ya Mongoroma  na kulia ni Kituo ch Afya Serya





Kushoto ni vyoo S/M Bolisa na kulia ni vyoo vipya vya S/M Bolisa





Kushoto ni nyumba ya mwalimu S/M Hachwi na kulia ni nyumba ya mwalimu S/M Hachwi





Kushoto ni madarasa S/M Kolowasi kulia ni madarasamapya S/M Kolowasi

# MIRADI MINGINE ILIYOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU





Kituo cha Afya Serya



Jengo la mochwari Hospitali ya Mji



Zahanati ya Hachwi



Madarasa Kondoa Girls



Zahanati ya Ausia



Kituo cha Afya Kolo



Madarasa ya awali